1.MATUMIZI NA UFAHAMU.

Tafadhali soma Vigezo na Masharti haya ('Masharti ya Matumizi').

Vigezo na Masharti haya ('Masharti ya Matumizi ') vinanapatikana kwa Watumiaji wa Huduma ya Maboto Microfinance na vitahusika mara moja unapojiunga au kujiandikisha na huduma ya Maboto Microfinance kupitia USSD *148*18# ('Huduma').

Mikopo ya Maboto Microfinance kupitia USSD *148*18 inatolewa kwa wateja ambao ni watumishi wa serikali wenye kutumia mitandao wa Vodacom pamoja na M-pesa, Airtel Money Pamoja na Tigopesa ambao wanaopatikana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuzingatia Masharti ya Matumizi haya.

Maboto Microfinance mara kwa mara itahakikisha, nyaraka zako za utambulisho au kurekebisha Masharti ya Matumizi haya au kutathmini/kupitia upya kikomo chako cha mkopo. Maboto Microfinance wanahaki ya kukubali au kukataa ombi lako la mkopo.

2.FAFANUZI NA TAFSIRI.

2.1 'Mkataba' maana yake ni Masharti ya Matumizi

2.2'Mkopo wa Maboto Microfinance au Huduma ya Mkopo au Huduma' maana yake ni huduma ya fedha ya kieletroniki ya simu ambayo inawawezesha wateja wa Maboto Microfinance kupata huduma ya upataji fedha ili kukidhi mahitaji binafsi na fedha hii italipwa na mteja ndani ya muda aliouchagua pamoja na riba na ad azote zilizoainishwa au kukatwa moja kwa moja kutoka kwa muajiri wake siku ya mshahara.

2.3 MABOTO MICROFINANCE Limited" ni kampuni ambayo Ofisi zake zipo Barabara ya Nyasaka, S.L.P 10316, Mwanza.

2.4 BOT maana yake ni Benki Kuu Ya Tanzania.

2.5 Mteja au Wateja wa Maboto Microfinance maana yake ni mtumiaji yeyote wa Maboto Microfinance ambaye amesajiliwa kutumia huduma ya Maboto Microfinance na ameingia kwenye makubaliano haya.

2.6 Kituo cha huduma kwa Wateja" maana yake ni kituo maalumu cha huduma ya mteja kwa mujibu wa mkataba huu.

2.7 Tukio la ukiukwaji' linamaanisha hali yoyote iliyohainishwa katika kifungu cha 9 hapo chini.

2.8 USSD *148*18# ni namba ya kutoa huduma za Maboto microfinance

2.9 Upataji Mkopo' au 'Mkopo' maana yake ni upataji wa mkopo unahohusishwa na mwenendo wako wa marejesho ya mikopo kutokana na taarifa zinazopatikana CRB Pamoja na kiwango chako cha mshahara kama mtumishi wa serikali.

2.10 Viwango vya Mkopo maana yake ni kiwango cha juu cha upataji Mkopo ambacho Mteja anaweza kutumia kwa mwezi.

2.11 Ada' maana yake ni tozo zinazotumika kwa huduma na ni pamoja na;

- 2.11.1Ada ya Uchakataji: (kama ilivyoainishwa kwenye viwango vya ada)
- 2.11.2 Malipo haya yatakatwa kila mteja anapoomba huduma ya Mkopo na MABOTO MICROFINANCE kikamilifu.
- 2.11.3Ada ya kinga ya mikopo chechefu (mikopo isiyolipika)
- 2.11.4 Hii ni ada kulingana na muda au idadi ya siku ambayo mteja atastahili kulipa kulingana na kiasi anachodaiwa.
- 2.11.5 Malipo mengine yoyote ya upataji Mkopo kama yalivyohainishwa mara kwa mara kwa mujibu wa mkataba huu na inajumuisha gharama zozote, na kodi zinazohusika chini ya Sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.12 Tukio la Ukiukwaji' maana yake ni

- 2.12.1 Hali ambapo upataji wa Mkopo umekamilika na haujalipwa kwa siku thelathini (30) au zaidi na kuwa mkopo chechefu,
- 2.12.2 Iwapo umefanya uvunjaji wowote au kushindwa kuzifata au kutekeleza, vigezo, maagano ya masharti au masharti ya makubaliano yoyote kati yetu na wewe mwenyewe kuhusiana na upataji wa Mkopo; au
- 2.12.3 Ikiwa kuna wasiwasi au hofu kwamba hutaweza kulipa madeni yako au tunapokea taarifa yoyote kwamba umekubali kutokuwa na uwezo wowote wa kulipa madeni yako kama ilivyokusudiwa.

2.13 Muda wa Kulipa Mkopo' maana yake ni pale mbapo hakuna tukio la ukiukwaji (kama ilivyoelezwa katika Mkataba huu) ndani ya siku ya thelathini (30) tangu tarehe ya kwanza ya matumizi ya Upataji Mkopo.

2.14 Serikali' ina maana serikali ya taifa, serikali kuu au Serikali nyingine yoyote iliyowekwa chini ya sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.15 Jua Wateja Wako' pia inajulikana kama KYC ni matakwa yaliyowekwa kisheria dhidi ya Maboto Microfinance Limited yanayohusu kumjua na kumfanyia upembuzi yakinifu mteja kama ilivyoainishwa kuagizwa au kupendekezwa na Serikali, Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) au Benki Kuu ya Tanzania (BOT) mara kwa mara.

2.16 MABOTO MICROFINANCE maana yake ni huduma ya kifedha ya mkopo na malipo ambayo inasimamiwa na kuendeshwa kipekee na Maboto Microfinance Limited nchini Tanzania na kuidhinishwa/kupewa kibali na Benki Kuu ya Tanzania

2.17 Akaunti ya MABOTO MICROFINANCE" maana yake ni mfuko maalumu wa MABOTO MICROFINANCE uliosajiliwa na unaokuwezesha kujiunga kwenye huduma ya Mkopo.

2.18 Taarifa za utambulisho wa Mteja" maana yake ni jina la mtumiaji wa MABOTO MICROFINANCE kama mtumishi au muajiriwa wa serikalini au mashirika ya umma; nambari ya utambulisho kazini (check number) kadi ya utambulisho ya kitaifa, nambari ya kadi ya mpiga kura, namba ya pasipoti/hati ya kusafiria au namba ya leseni ya kuendesha gari, kama inavyoonekana mara kwa mara katika mifumo ya Maboto Microfinance.

2.19 Mfumo wa MABOTO MICROFINANCE maana yake ni mfumo unganishi wa kiufundi kwa sasa hivi unaotoa huduma ya mikopo

2.20 Check number" maana yake ni namba ya utambulisho wa mpokea mshahara au malipo ya serikali au mtumiaji au mtumishi wa serikali au mashirika ya umma.

2.21 USSD maana yake teknolojia ya mawasiliano yenye mfumo wa kimataifa wa mkononi (GSM) ambayo hutumiwa kutuma ujumbe kati ya simu za mkononi na mfumo maalum wa mtandao. Maombi yanaweza kujumuisha matumizi kabla ya kulipia au huduma za kuzungumza na simu zinazotolewa na Maboto Microfinance Limited

2.22 Masuala ya Kiupembuzi ya Mteja"maana yake ni nyaraka za kibinafsi zinazotolewa na mtumishi kuja kwetu kwa nia ya kuthibitisha jina lako na anwani ya sasa na mahala pa kuajiriwa, ili kufikia mahitaji yetu ya kisheria ya kudhibiti.

2.23 Ukurasa wa Tovuti au Tovuti maana yake ni kikundi cha kurasa kilichounganishwa kwenye habari za mtandao juu ya somo fulani k.m. www.maboto.co.tz

2.24 Mtandao maana yake ni mfumo wa kimataifa wa mawasiliano wa simu za mkononi ('GSM') mfumo unaondeshwa na Makampuni ya simu za mikononi na kufika maeneo ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania

2.25 Matatizo Yasiyozuilika' maana yake ni kitu chochote kisichokuwa na udhibiti wa mtu yeyote yule, ikiwa ni pamoja na majanga, kitendo cha vita au ugaidi, uhamasishaji wa majeshi ya kivita, usumbufu wa kiraia au machafuko, maafa ya asili, maandamano au usumbufu wa kazi (achilia mbali maandamano ya wafanyakazi wa mhusika yoyote wa mkataba huu au washirika wake), kizuizi cha sarafu, kizuizi, au kusitishwa kwa huduma za umma au kushindwa kwa usambazaji wa mawasiliano ya simu au kushindwa kwa mfumo, ucheleweshaji katika uchakataji wa miamala, au ucheleweshaji uliopo nje ya uwezo wetu wa kawaida (ni pamoja na kushindwa kwa nguvu za umeme na kucheleweshaji katika mawasiliano na uuzaji katika vituo husika, mtandao au mfumo mwingine na ni pamoja na kushindwa kwa kifaa chako).

2.26 Sisi, yetu, na nasi inamaanisha Maboto Microfinance Limited na (ikiwa inafaa) Msaidizi;

2.27 "Wewe" au "yako" au "nawe" au "mtumishi" maana yake ni mteja na hujumuisha wawakilishi binafsi wa Mteja

2.28 Maneno yanayowakilisha umoja au wingi yatakuwa sawa na yanaweza kutumika kwa pamoja.

3.KUKUBALI VIGEZO NA MASHARTI

3.1 Kabla ya kuingia au kujiunga na huduma hii, unapaswa kusoma kwa uangalifu na kuelewa masharti haya ya matumizi yanayosimamia upatikanaji wa matumizi na uendeshaji wa Huduma. Masharti haya ya Matumizi yanapatikana kwenye tovuti yetu www.maboto.co.tz

3.2Kama hukubaliani na masharti ya matumizi haya, tafadhali bonyeza 'Sitisha' kwenye huduma ya kujiunga.

3.3 Kwa kuomba mkopo kwa njia ya USSD *148*18# utakuwa umeisoma, umeelewa na kukubali Masharti ya Matumizi: Kwa kubonyeza chaguo 'Kukubali' wakati wa kujiunga pale inapokuomba uhakikishe kuwa umesoma, umeelewa na umekubali kutekeleza vigezo na masharti haya na utakuwa umekubali masharti ya matumizi pia kwa kutumia au kuendelea kutumia na huduma ya Maboto Microfinance.

3.4 Kwa kujiandikisha kwa Huduma hii, unakubali kuzingatia na kufuata masharti ya matumizi haya kama yatakavyokuwa yanafanyiwa marejeo na kurekebishwa mara kwa mara na unathibitisha kuwa vigezo na masharti hayaathiri haki nyingine yoyote ambayo tunaweza kuwa nayo kisheria au vinginevyo kuhusu usajili wako, upatikanaji na matumizi ya huduma.

4.KUJIUNGA NA MATUMIZI YA HUDUMA

4.1 Huduma hii inapatikana kwa Watumishi wa serikali tu kwa kupitia *148*38# na kwa kufanya hivyo ina maana kwamba umeridhia masharti na matumizi haya.

4.2 Maboto Microfinance inahaki ya kuthibitisha uhalali wako pia ina uhuru wa kusitisha/kukataa maombi yako kwa taarifa au bila taarifa, ingawaje (itambulike kuwa sio wajibu wetu kukujulisha) tunaweza jaribu kukujulisha.

4.3 Unaweza kujiandikisha na huduma kwa zaidi ya mtandao mmoja ingawaje masharti ya matumizi yatatumika kwa kutumia check number yako.

4.4 Unakubali na kutoa mamlaka kwa Maboto Microfinance Limited kupata na kutumia taarifa zako binafsi kulingana na utoaji wa huduma hii. Maelezo hayo kibinafsi yanajumuisha bila ya kikomo, pamoja na nambari yako ya simu, jina, tarehe ya kuzaliwa, aina ya kitambulisho na nambari yake na taarifa nyingine zitakayotuwezesha kutambua na kufuatilia na kukidhi mahitaji ya udhibiti wa 'Jua Wateja wako(KYC)'.

4.5 Pia unakubali na kuturuhusu kutumia habari zinazohusiana na matumizi yako ya Mtandao wa simu kwa madhumuni ya kutoa huduma

4.6 Maboto Microfinance tuna haki ya kuomba taarifa zaidi kutoka kwako kuhusiana na maombi yako ya kujiandikisha kwa huduma wakati wowote. Kushindwa kutoa maelezo kama hayo wakati tunahitaji kunaweza kusababisha kusitishwa kwa maombi yako ya kujiasajili kwenye huduma.

4.7 Kukubali au kukataa kwa maombi yako kujisajili kwenye huduma utafanyika kwa kupitia ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) itakayo tumwa kupitia namba yako ya simu iliyosajiliwa na muajiri wako dhidi ya Check number yako na inayohusishwa na akaunti yako ya MABOTO MICROFINANCE USSD na au vifaa vingine.

4.8 Kwa kukubali Vigezo na Masharti haya, unakubali na kuthibitisha kwamba tuna haki ya msingi na ya kipekee ya kuweka kiwango cha Mkopo na/au ada yoyote / makato yanayohusiana na huduma hii.

4.9 Unaweza kutumia tu upataji wa Mkopo ili kukamilisha matumizi au mahitaji binafsi

4.10 Utapata taarifa kukubali upataji wa Mkopo pindi unapokamilisha maombi yaliyokubaliwa pamoja na ada zote kulingana na masharti ya matumizi.

4.11 Kwa kukubali Vigezo na Masharti haya, unakubaliana na kukiri kwamba tunahaki ya pekee ya kukutuma ujumbe wa maandishi ya matangazo mara kwa mara kuhusiana na huduma.

5.VIWANGO VYA MKOPO / VIWANGO VYA MKOPO NA MABOTO MICROFINANCE USSD

5.1 Baada ya kuingia kwenye Huduma, utapokea ujumbe wa uthibitisho ulio na kiwango cha Mkopo.

5.2. Unaweza kuangalia kiwango cha Mkopo kwa kutumia chaguo sahihi la orodha iliyopo kwenye Simu yako / kwenye vifaa vyako kupitia Maboto Microfinance USSD.

5.3 Mara kwa mara tunaweza kukupangia kiwango cha juu au cha chini cha Mkopo iwapo umeomba huduma hiyo, na kiwango hicho kitawasilishwa kwako kupitia ujumbe mfupi wa maneno (SMS)

5.4. Viwango vya Mkopo vinaweza kupitiwa mara kwa mara na tunahaki ya kupitia tena na kutofautisha viwango vya Mkopo kwa taarifa au bila kutoa taarifa; ingawa (siyo wajibu wetu) tutajaribu kukupa taarifa kuhusu utofauti wowote wa viwango vya Mkopo pale itakapobidi.

6.KUOMBA UPATAJI WA MKOPO

6.1Unakubali kwamba upataji wa Mkopo utapelekea deni kulingana na dhamani ya kiwango cha Mkopo na ada zote stahiki.

6.2 Ada zote zitajumuhishwa kwenye kiwango cha Mkopo na zitalipwa kupitia rejesho la muda uliouchagua. Ada zitajumuisha ushuru na kodi yoyote inayotambulika, zinazotumika chini ya sheria.

6.3 Kwa kiwango cha Mkopo ulichopata, unapaswa kulipa chote ndani ya siku 7 au 14 au 21, na isizidi siku ya thelathini (30) tangu tarehe ambapo umepata Mkopo (tarahe ya kwanza ya kupata Mkopo). Hutaweza Kupata Mkopo mpya au kuongeza nyingine ikiwa una deni la awali au umekiuka masharti na matumizi ya Mkopo

6.4 Unaweza kuomba huduma ya Mkopo mara nyingi uwezavyo ndani ya kipindi cha malipo ili mradi maombi hayo hayatazidi kiwango cha Mkopo ulichoruhusiwa. Ili kupata Mkopo ya pili, ni lazima uwe tayari umelipa Mkopo wa awali.

6.5 Kulingana na mwenendo wako kwenye Maboto Microfinance na huduma ya Mkopo, viwango vya Mkopo vinaweza kuongezwa au kupungua. Utendaji mzuri unaweza kusababisha ukuaji wa kiwango cha Mkopo. Utendaji mbaya unaweza kusababisha kupungua kwa kiwango cha Mkopo au kusitisha kabisa.

6.6 Huwezi kupata Mkopo zaidi ya kiwango chako cha juu katika mshahara wako. Ingawa inaweza kutokea ukapata huduma ya Mkopo au kupata kiwango kikubwa zaidi ya kile ulichoruhusiwa. Iwapo hali hii itatotekea, utalazimika kutulipa kwa mujibu wa masharti ya matumizi haya.

7.UKOKOTOAJI WA KIWANGO CHA MKOPO

7.1 Mifumo ya kipembuzi ya Maboto Microfinance Limited itatumika kutoa alama ambazo zitaamua kiwango cha Upataji Mkopo

7.2.Kiwango cha Mkopo na muendelezo wa uidhinishaji wetu wa maombi yako ya Mkopo kitaamuliwa na alama za kiupembuzi za Maboto Microfinance Limited. Mfumo wetu utafanya mahesabu ambayo itaamua kiwango chako cha Mkopo ambacho kimetokana kulingana na masuala mbalimbali ambayo bila kikomo ni pamoja na kipato chako, Huduma za Maboto Microfinance na historia ya ulipaji wa madeni kutoka kwenye Credit Reference Bureau (CRB).

8.REJESHO LA MKOPO

8.1 Kiwango cha Mkopo ulichopata kinapaswa kulipwa chote ndani ya siku 7 au 14 au 21, na isizidi siku thelathini (30) tangu tarehe ambapo umepata Mkopo (tarahe ya kwanza ya kupata Mkopo). Hutaweza kupata Mkopo mpya au kuongeza nyingine ikiwa una deni la awali au umekiuka masharti na matumizi ya Mkopo

8.2 Baada ya kuchukua huduma ya Mkopo, Taarifa za deni lako zitawekwa kwenye huduma ya ufuatiliaji madeni. Huduma ya kukatwa moja kwa moja kutoka kwenye mshahara wako itafanyika tu pale deni lako litakapopitisha siku 30. Hii inamaanisha kuwa Maboto Microfinance Limited itatuma taarifa kwenda kwa muajiri wako ili deni likatwe moja kwa moja kutoka kwenye mshahara wako na kulipa kwenye akaunti yako ya Maboto Microfinance kupitia deduction code number 733 wakati wote hadi pale ambapo kiwango chote cha Mkopo ulichopewa kimerejeshwa kikamilifu.

- 8.2.1 Kwanza utalipa ada zote zinazohitajika.
- 8.2.2 Pili utalipa rejesho lote la Mkopo.
- 8.3 Baada ya kupita kwa muda wa Mkopo, Maboto Microfinance inahaki ya kuhuisha ama kuongeza muda wa kulipa Mkopo. Kwa mujibu/kadri ya mapitio yetu ya mara kwa mara ya kikomo chako kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 5, unakubali kuwa kukokotoa upya ama kuendeleza upataji wa mikopo ni sehemu ya vigezo na masharti yaliyomo humu. Utapata taarifa kila mara muda wa kulipa Mkopo utakapohuishwa au kuongezwa.

9.MATOKEO YA UKIUKWAJI

9.1 Wakati wowote baada ya tukio la ukiukwaji limetokea, tuna haki ya:

- 9.1.1Kusitisha huduma kwa taarifa au bila taarifa au kwa mujibu wa kifungu cha 13 chini;
-

9.1.2 Kuamuliwa kulipa mara moja Kiwango chote Cha Mkopo (ikiwa ni pamoja na ada na gharama zote) na kiasi kingine chochote kilichopo chini ya Masharti na Matumizi haya, ambapo unawajibika kulipa na;

- 9.1.3 Unaturuhusu sisi kuwasilisha taarifa yako (yaani Tukio la Ukiukwaji) ya mikopo kwa taasisi za kutunza kumbukumbu za mikopo kulingana na matakwa ya sheria ya mabenki na taasisi za kifedha au kwa taasisi zingine za kiudhibiti.
- 9.1.4 Kutoa taarifa kwa muajiri wako ili makato ya deni kufanyika moja kwa moja kupitia Deduction code 733. Endapo hii itashindikana, kuhusisha taasisi za ukusanyaji mikopo ili kuwezesha urejeshaji wa kiwango/madeni yaliyokiukwa.

10.ADA, MAKATO NA GHARAMA

10.1 Unawajibika kwa malipo ya ada zote zinazotokana na matumizi ya huduma.

10.2 Ada zote zinakatwa mwanzoni mwa maombi na zinaweza kubadilika wakati wowote pindi tutakavyoona inafaa.

10.3 Ada zinazolipwa chini ya Mkopo zitawekwa kwenye rejesho lako. Kwa hiyo unakubali kwamba endapo hutafanya marejesho kulingana na makubaliano, Maboto Microfinance inahaki ya kukata kutoka kwenye mshahara wako na malipo yafanyike kupitia deduction code 733 (bila kukutaharifu) ada yoyote ya miamala inayolipwa inatokana na huduma hii;

10.4 Isipokuwa kama inavyofahamika vinginevyo, ada zinajumuisha kodi zote zinazohusika pamoja na kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha juu. Mteja unakubali kulipa ada zote za miamala.

10.5 Unakubali kulipa gharama zote zilizotumika na sisi katika kupata au kujaribu kupata malipo /rejesho unayodaiwa.

10.6 Unapaswa kukamilisha ombi lako la Upataji wa Mkopo kwa ufanisi kila mara unapoomba huduma ya Mkopo.

10.7 Ada zote zinazohusiana na matumizi yako ya huduma ya MABOTO MICROFINANCE zitakuwa chini ya mujibu wa Masharti ya Matumizi ya huduma.

11.KODI

11.1 Marejesho yote yatajumuisha ushuru wowote unaolipwa kama inavyotakiwa na sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

11.2 Bila pingamizi lolote lile, unatupa ruhusa ya kufanya marekebisho ya ada pale ambapo kutatokea mabadiliko yoyote ya sheria za kodi.

12.MATUMIZI YA TAARIFA BINAFSI

12.1 Kwa hivyo unakubali kwa dhati na umetuidhinisha sisi (Maboto Microfinance Limited) kupokea,kutoa taarifa zako au kutumia taarifa zako binafsi au habari au data inayohusiana na namba yako ya simu Pamoja na Check number yako kuhusu upataji Mkopo uliyopewa chini ya huduma hii na maelezo yoyote juu ya matumizi yako ya huduma kwa;

- 12.1.1 Kwenda na kutoka kwa watoa huduma zetu, wafanyabiashara, mawakala au kampuni nyingine yoyote ambayo inaweza kuwa washirika wetu au kampuni tanzu au kampuni mama kwa madhumuni ya kibiashara yanayohusiana na huduma;
- 12.1.2 Kwa Taasisi Kumbukizi za Mikopo (Credit Reference Bureau);
- 12.1.3 Kwa taasisi huru za ukusanyaji wa mikopo;
- 12.1.4 Kwa wanasheria wetu, wakaguzi au washauri wengine wa kitaalam au kwa mahakama yoyote au mahakama ya usuluhishi kuhusiana na kesi yoyote ya kisheria au ukaguzi;
- 12.1.5 Kwa madhumuni ya kibiashara yenye kuhusiana na matumizi yako ya huduma, kama uuzaji na shughuli zinazohusiana na utafiti; na
- 12.1.6 Katika mazoea ya kibiashara pamoja na bila kufungamana na udhibiti wa ubora, mafunzo na kuhakikisha uendeshaji mzuri wa mifumo.

12.2 Unatuidhinisha kutoa habari yoyote inayohusiana na mikopo yako kupitia MABOTO MICROFINANCE kwa mamlaka ya sheria yoyote ndani ya nchi au mashirika ya serikali ili kusaidia katika kuzuia, kugundua, uchunguzi au uendeshaji mashtaka ya jinai au udanganyifu au kwa taasisi nyingine yoyote au washiriki kama inavyotakiwa na sheria za nchi yoyote na kadiri tunavyoona ni muhimu.

12.3 Unatuidhinisha kutoa, kujibu, kushauri, kubadilishana na kuwasilisha maelezo au habari zinazohusiana na mkopo wako na MABOTO MICROFINANCE na / au Upataji Mkopo kwa watu wengine/washiriki wanaohusika katika usimamizi wa madeni na upataji Mkopo, usafishaji wa kanzidata(database), au utoaji ya msaada wa watumiaji.

13.MABADILIKO, USIMAMISHAJI NA USITISHAJI

13.1 Tunaweza wakati wowote, kusitisha au kutofautisha uhusiano wetu wa kibiashara na wewe au kuzuia usajili wako na au upataji Huduma:

13.1.1 Iwapo unatumia Huduma hii kwa madhumuni yasiyoruhusiwa au tunagundua matumizi mabaya, uvunjaji wa yaliyomo, udanganyifu au kujaribu kudanganya matumizi yako ya huduma;
13.1.3 Ikiwa Check number yako imesimamishwa kwa sababu yoyote;
13.1. Ikiwa tunahitajika au kuombwa kufuata, tii/kuzingatia agizo la au pendekezo kutoka kwa serikali, mahakama, mdhibiti au mamlaka nyingine inayofaa kwa tahadhari hiyo au umuhimu huo;
13.1.5 Ikiwa tunashuku au tunaamini kuwa unakiuka masharti ya matumizi (pamoja na kutokulipa malipo yoyote unayodaiwa);
13.1.6 Ambapo Check number yako inakuwa haifanyi kazi au mfu au inachukuliwa kuwa imesitishwa.
13.1.7Ikiwa tutaamua kusimamisha au kusitisha utoaji wa huduma kwa sababu za kibiashara au kwa sababu nyingine yoyote kama itakavyoamuliwa.

13.2 Unaweza kufuta (i.e. kutengua) usajili wa huduma wakati wowote kupitia vifaa vyako; Ila hutaweza kutengua usajili ikiwa una Mkopo au unadaiwa rejesho au ada zozote zile.

13.3 Usitishaji huduma hakutaathiri haki na majukumu yoyote ya kisheria kwa pande yoyote ile na, haswa, haitaathiri majukumu yako ya kukidhi ulipaji deni lolote lililopatikana kabla ya kusitisha huduma.

13.4 Tunaweza kusitisha uhusiano wetu na wewe na kusimamisha upatikanaji wa huduma ikiwa utashindwa kulipa Mkopo pamoja na ada yoyote unayodaiwa ndani ya muda wa kulipa Mkopo ambao ni siku thelathini (30).

13.5 Ikiwa unadaiwa salio la Mkopo kwa zaidi ya siku thelathini (30), haki yako ya kutumia huduma ya Mkopo na Maboto Microfinance itasitishwa mara moja mpaka utakapo fanya malipo ya Mkopo,na mpaka pale marejesho ya kiwango yatakapofanyika.

14.MABADILIKO YA VIGEZO NA MASHARTI

14.1Tunaweza kuongeza au kubadilisha masharti ya matumizi wakati wowote kwa hiari yetu. Tunaweza kuongeza ada mpya na makato au kubadilisha ada zilizopo wakati wowote;iwapo kutatokea matokeo ya moja kwa moja ya sheria mpya, chombo cha kisheria, kanuni au leseni za Serikali, uwekaji au mabadiliko ya kodi za serikali au mapitio yoyote ya kimkakati ya mipango ya biashara ya Maboto Microfinance Limited, mabadiliko ndani ya tasnia ya mawasiliano, mapendekezo kutoka kwa vyombo vya kisheria au kwa sababu yoyote ile kama tunavyoweza kuamua kwa hiari yetu.

14.2 Tutajaribu kukujulisha mapema ikiwa tunaongeza au kubadilisha masharti ya matumizi. Kiwango na aina ya taarifa ambayo tutakupa itafuata njia muhimu inayotumika na inayopatikana wakati huo. (Kwa mfano, tunaweza kukujulisha kwa barua, barua ya elektroniki, simu (pamoja na ujumbe uliorekodiwa au ujumbe wa simu) au kwa tangazo katika gazeti la kila siku au gazeti la kila wiki au kwenye tovuti yetu au njia nyingine yoyote). Mabadiliko hayo yatatokea kabla au baada ya kukuambia juu ya hilo, unashauriwa pia kutembelea tovuti yetu mara kwa mara ili kuona mabadiliko iwapo hujapata taarifa hizo kwa sababu yoyote ile iliyo nje ya uwezo wetu.

15.KWA UJUMLA

15.1Vigezo na Masharti haya (kama yanavyoweza kurekebishwa mara kwa mara) ni makubaliano ya kisheria yanayokubana wewe binafsi pamoja wawakilishi wako wa kibinafsi.

15.2 Hatutawajibika kwa kucheleweshaji au kushindwa kutekeleza majukumu yetu yanayohusiana na utumiaji wa huduma ya Mkopo kupitia *148*18# iwapo ucheleweshaji huo au kushindwa huko kumesabishwa na sababu au hali yoyote iliyo nje ya uwezo wetu au kwa sababu ya matatizo yasiyozuilika.

15.3 Hauwezi kubadilisha kwa namna yoyote masharti ya matumizi na hauwezi kuhamisha majukumu haya kwa mtu mwingine yeyote au biashara.

15.4 Mkataba huu utasimamiwa na kutafasiriwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

15.5Mawasiliano yote chini ya mkataba huu yatakuwa kwa Kiingereza au Kiswahili.

15.6 Masharti ya Matumizi haya hayasitishi Masharti yoyote ya Matumizi na yatasomwa kwa kushirikiana na kanuni na masharti ya wateja wa Maboto Microfinance.

16.MAWASILIANO NA MALALAMIKO

16.1 Ikiwa haujaridhika na huduma yoyote inayotolewa, tafadhali wasiliana na Kituo cha huduma kwa mteja wa Maboto Microfinance kwa kupiga simu namba 0656506606 au 0764225366. Tutaoa ushirikiano wa kutatua lalamiko lako na kukuelezea utaratibu wa malalamiko kwa undani zaidi. Tutajaribu kutatua malalamiko yako haraka iwezekanavyo. Mara nyingi hata hivyo, malalamiko yatahitajika kuchunguzwa. Ikiwa hali ndio hii, tutakujibu ndani ya siku 5 za kazi na tutakiri kupokea malalamiko yako na tunaweza kukujibu itachukua muda gani ili malalamiko yako kutatuliwa. Ikiwa malalamiko yako hayawezi kutatuliwa utashauriwa ipasavyo.

ADA NA VIWANGO VYA MKOPO

Riba inayotumika kwa asilimia tatu nukta tano (3.5%) kulingana na salio la deni (reducing balance).

Unapotumia huduma ya Mkopo utalipa gharama ya ada ya maombi: kulingana na kiwango unachopewa. Ada hii itatozwa mara moja tu pale utakapotumia huduma ya Mkopo.

Viwango	**Ada ya Kinga (Indemnity)**
10000 - 100000	5%

Ada ya siku: ambayo hulingana na muda uliochagua kufanya marejesho.

Viwango	**Ada ya kila siku**				
	Siku 1 hadi 7	Siku 8 hadi 14	Siku 15 hadi 21	Siku 22 hadi 31	Siku 31 na Zaidi
10000 – 100000	5%	6%	7%	8%	10%